# NISHANI YA NYOTA

NA
SULEMANI MANGE
IDARA YA VIJANA
TANZANIA UNION
2007

1 Pr. S. Mange

# Dunia Inazunguka



•

2 Pr. S. Mange

# NISHANI YA NYOTA

- SEHEMU YA KWANZA

3 Pr. S. Mange

# Nishani ya Nyota

- Kwa nini tujifunze nishani ya nyota?
- 1. Ili kujua ukuu wa Mungu. Mungu ni mkuu mno na watu hatujui. Tukijua tutamhofu.
- Tukijifunza vitu alivyoviumba Mungu, tutatambua ukuu wake.

4 Pr. S. Mange

# Nishani ya Nyota

- Biblia inasema: ***"Tazama, Mungu ni mkuu, nasi hatumjui; Hesabu ya miaka yake haitafutiki"*** (Ayubu 38: 26). Tukijifunza ingawaje kidogo juu ya vitu alivyoviumba tutaongeza kumjua alivyo mkuu.

5 Pr. S. Mange

# Nishani ya Nyota

- Biblia inasema: ***"Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, na anga laitangaza kazi ya mikono yake"*** (Zab. 19:1). Tukijifunza aliyoyaumba Mungu tutaujua ukuu wa utukufu wake.

6 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mungu ameumba vitu vingi vidogo sana na vikubwa sana ambavyo watu wengi hawavijui kuwa vipo.
- 2. Tunajifunza nishani ya nyota ili kujua pande za dunia bila ya kutumia vyombo vinavyoonyesha pande za dunia.

7 *Pr. S. Mange*

## Nishani ya Nyota

- Kwa maelezo yangu:
- Nyota ni kitu kinachotoa
- nuru na joto, lakini hakiteketei.

8 *Pr. S. Mange*

## Nishani ya Nyota


Nyota inayojulikana na kila mmoja ni Jua.

- Jua ni kama nyota zote zilizopo angani.
- Inaonekana kubwa kwa sababu iko karibu
- Jua liko maili 93,000,000 toka duniani.

9 *Pr. S. Mange*

## Nishani ya Nyota

- Jua ni kubwa sana
nia.




**Kipenyo cha Jua ni maili 865,000**

10 *Pr. S. Mange*


## Nishani ya Nyota

- Jua limeumbwa kwa hewa ya:
- 1. Hydrogen, ambayo ni asilimia 75 ya mwili wa Jua.
- 2. Helium, ambayo ni asilimia 25 ya mwili wa Jua.
- Helium iko katikati ya mwili wa Jua.

11 *Pr. S. Mange*

## Nishani ya Nyota

- Jua limeumbwa kwa
na helium.




12 *Pr. S. Mange*

## Nishani ya Nyota

- Joto juu ya Jua ni nyuzi
  0 Centigrade.

**Joto la Jua juu yake ni kali sana, linayeyusha cho chote.**

13 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Joto katikati ya mwili wa Jua ni nyuzi joto
  ,000 Centigrade.
  kali sana.

**Joto katikati ya Jua ni kali halielezeki kabisa**

14 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- Jua linamlikia sayari tisa.
- Sayari hizo, kwa mfuatano ni:
- 1. Mercury (Zebaki)
- 2. Venus (Zuhura)
- 3. Earth (Dunia)
- 4. Mars (Mihiri) - Hizi ni sayari ndogo ndogo "Terrestrial Planets"

15 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Jua na sayari kadhaa kwa mfuatano.




16 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 1. MERCURY ina kipenyo cha maili 3,029.
- 1). Inachukua siku 59 kujizungusha kupata mchana na usiku.
- 2). Mercury huchukua siku 88 kulizunguka Jua.
- 3). Iko maili 36,000,000 toka kwenye Jua

17 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 2. VENUS ina kipenyo cha maili 7,521.
- 1). Inachukua siku 243 kujizungusha kupata mchana na usiku.
- 2). Venus huchukua siku 243 kulizunguka Jua.

3). Venus iko maili 67,000,000 toka kwenye Jua

18 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- 3. EARTH (Dunia), ina kipenyo cha maili 7,918.
- Inachukua masaa 24 kujizungusha kupata mchana na usiku.
- Dunia huchukua siku 365.25 kulizunguka Jua.
- Dunia iko maili 93,000,000 toka kwenye Jua

19 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- Dunia ikijizungusha huku ikisafiri kuzunguka Jua.



20 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota
## Dunia Inazunguka Jua



21 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Dunia ina viumbe aina 1,750,000
- Katikati ya Dunia kuna chuma na nickel iliyoyeyuka, kutokana na joto kali lenye nyuzi 5,000 centigrade. Baadaye, miamba.

22 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Dunia unazungukwa na utando wa hewa, “ozone layer”, iliyoumbwa kwa hewa ya Oxygen yenye atom tatu.
- Dunia ina “satellite” (Mwezi), moja ulio umbali wa maili 240,000.
- Mwezi hutumia siku 28 kuizunguka Dunia.

23 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Watu wa kwanza kufika mwezini ni: Neil Armstrong na Edwin Aldrin waliofika mwezini tarehe 16Julai 1969 na kukaa huko hadi tarehe 24 Julai 1969.
- Walisafiri kwa chombo kinachoitwa Apollo namba 11.

24 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mwezi huwa haujizungushi kupata usiku na mchana, sehemu moja ni mchana daima na nyingine ni usiku daima.
- Mwezi hutoa nuru usiku na nuru hiyo, unaakisi toka kwenye Jua.

25 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Sayari nyingine kwa mfuatano ni:
- Jupiter (Sumbula)
- Saturn (Sarateru)
- Uranus (Zohari)
- Neptune (Kausi)
- Sayari hizi nne ni kubwa kubwa "Jovian au Giant planets.

26 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- Mwezi haujizungushi ili kupata usiku na mchana.
- Hivyo, sehemu moja ni mchana na nyingine ni usiku milele zote.

27 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Jua na sayari zake tisa



28 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 4. MARS ina kipenyo cha maili 4,213.
- Mars huchukua masaa 24.36 kujizungusha ili kupata usiku na mchana.
- Mars iko umbali wa maili 141,000,000 toka kwenye Jua.

29 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mars ina satellites mbili, Phobos na Deimos, satellites ndogo kuliko Mwezi.

30 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Sayari ya Mars inaitwa "Sayari Nyekundu" kwani ina majangwa

31 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Joto la Mars linazidi kidogo nyuzi 0, na usiku linafikia -125 centigrade.

32 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Katikati ya Mars na Jupiter, kuna vimondo vidogo vidogo, (asteroids) vipatavyo million moja.

33 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kuna vimondo vikubwa vinne, vinavyoitwa:
- 1.Ceres - kina kipenyo cha maili 600.
- 2. Pallas
- 3. Hygiea
- 4. Vesta

34 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 5. JUPITER ina kipenyo cha maili 88,846.
- Ni moja ya sayari kubwa, (Jovian au Giant Planets).
- Jupiter hutumia masaa 9.92 kujizungusha ili kupata usiku na mchana.

35 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Jupiter hutumia miaka 11.8 kulizunguka Jua.
- Jupiter ni sayari kubwa kuliko sayari zote tisa zinazomlikiwa na Jua.

36 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Jupiter ina "satellite" 16.
- Jupiter iko umbali wa maili 483,000,000 toka kwenye Jua.

37 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 6. SATURN ina kipenyo cha maili 74,898.
- Saturn ni moja ya sayari kubwa "Jovian" au "Giant Planets"
- Saturn hutumia masaa 10.6 kujizungusha ili kupata usiku na mchana.

38 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Saturn hutumia miaka 29.4 kulizunguka Jua.
- Saturn ina "satellite" 18.
- Saturn iko umbali wa maili 1,432,000,000 toka kwenye Jua.

39 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Saturn ina utepe kwenye Ikweta yake ulioumbwa kwa theluji na kiasi fulani cha mavumbi na mawe.

40 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 7. URANUS ina kipenyo cha maili 31,763.
- Uranus ni moja ya sayari kubwa "Jovian" au "Giant Planets"

41 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Uranus hutumia masaa 17.24 kujizungusha ili kupata usiku na mchana.
- Uranus hutumia miaka 84.1 kulizunguka Jua.
- Uranus ina "satellite" 17.

42 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Uranus iko umbali wa maili 1,784,000,000 toka kwenye Jua.

43 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 8. NEPTUNE ina kipenyo cha maili 30,775.
- Neptune ni moja ya sayari kubwa "Jovian" au "Giant Planets"

44 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Neptune hutumia masaa 16.1 kujizungusha ili kupata usiku na mchana.
- Neptune hutumia miaka 164.9 kulizunguka Jua.

45 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Neptune ina "satellite" 8.
- Neptune iko umbali wa maili 2,795,000,000 toka kwenye Jua.

46 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 9. PLUTO ina kipenyo cha maili 1,432.
- Pluto ni moja ya sayari ndogo "Terrestrial Planet".
- Pluto hutumia masaa 6.4 kujizungusha ili kupata usiku na mchana.

47 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Pluto hutumia miaka 248.6 kulizunguka Jua.
- Pluto ina "satellite" 1.
- Pluto iko umbali wa maili 3,675,000,000 toka kwenye Jua.

48 Pr. S. Mange

Nishani ya Nyota

- Jua ni kubwa kuliko sayari zote tisa zikiwekwa pamoja.
- Sayari zote tisa hazina viumbe isipokuwa sayari yetu "Earth" au Dunia.

49 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Sayari zote huzunguka Jua kwa utaratibu zilizowekewa na Mungu wala hakuna sayari inayoacha utaratibu huo au kuingilia mstari (orbit) wa sayari nyingine.

50 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

*SEHEMU YA PILI*
*NA*
- *PR. SULEMANI MANGE*

51 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- Japo Jua ni kubwa namna hiyo, linasafiri kuelekea nyota ya Vega kwa kasi ya maili 200 kwa sekunde.

52 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Jua likisafiri maili 200 kuelekea Vega.




53 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Jua linaposafiri kuelekea nyota ya Vega, linasafiri pamoja na sayari zako zote, maana zimefungwa kwenye uvutano mmoja, bila kuvuruga umbali kati ya sayari na sayari.

54 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Jua linauvutano unaozishirikilia sayari zote.
- Mungu ni mkubwa sana, uwezo wake haueleweki.

55 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

1. BWANA Mungu, nashangaa kabisa
   Jinsi wewe ulivyo Mkuu mno
   Nyota, ngurumo, vitu vingi vyote
   Viumbwavyo kwa uwezo wako.

56 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 2. Nikitembea pote duniani,
  Ndege huimba nawasikia,
  Milima hupendeza macho sana,
  Upepo nao nafurahia.

Roho yangu na ikuimbie,
Jinsi wewe ulivyo Mkuu X2. 57 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

3. Nikikumbuka jinsi wewe Mungu,
   Ulivyompeleka Mwanao,
   Afe azichukue dhambi zetu,
   Kuyatambua ni vigumu mno.
   Roho wangu na ukuimbie,
   Jinsi wewe, ulivyo mkuu X2

58 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota


4. Yesu Mwokozi atakaporudi,
   Kunichukua kwenda Mbinguni,
   Nitashukuru na kuimba milele,
   Wote wajue jinsi ulivyo.

Roho yangu na ikuimbie,
Jinsi wewe ulivyo Mkuu X2. 59 Pr. S. Mange

Nishani ya Nyota
MFUNGAMANO WA NYOTA (Galaxy).

Nyota jirani na Jua inaitwa <u>Alpha Centauri.</u>

Iko umbali wa maili trillion 24.




60 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Maili Trillion 24 ni mbali sana. Biblia inaongea umbali wa nyota kwa kusema: *"Je! Mungu hayuko mbinguni juu? Tena tazama umbali wa nyota, jinsi zilivyo juu!" (Ayu.22:12).*

61 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Nyota ya pili jirani na Jua inaitwa Barnard's Star iko umbali wa maili trillion 30 kutoka kwenye Jua.


62 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Hadi sasa, tunajua nyota tatu:
- 1. Sun (Jua).
- 2. Alpha Centauri.
- 3. Barnard's Star.

63 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota




64 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Barnard's Star ni nyota iliyo na vipande vitatu viwili vidogo vikizunguka kile kikubwa.
- Nyota aina hizo zinaitwa Multiple Star.

65 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- Nusu ya nyota zilizo angani ni Multiple Stars kama ilivyo Barnard's Star.
- Mungu ni mwenye uwezo wa kuumba vitu aina nyingi.

66 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Barnard’s Star ambayo ni Multiple star.



67 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Barnard’s Star inaonekana kwa kiona mbali (telescope) ikizungukwa na sayari mbili kubwa zenye ukubwa kama wa Jupiter.

68 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kwa kawaida, kila nyota inamlikia sayari na sayari hizo zote, zina watu watakatifu.

69 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Watu wa kwenye sayari hizo hawakuangushwa dhambini na Shetani, hivyo ni watu watakatifu.

70 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Ellen White kwenye njozi alipelekwa kwenye sayari moja zinazomlikiwa na moja ya nyota za angani.

71 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Ellen White alikuta watu kwenye sayari hivyo, wazuri, wachangamfu, na alipowauliza ni kwa nini wao ni tofauti na watu wa Duniani, walimwambia kuwa wao hawajala tunda la ujuzi wa mema na mabaya kama watu wa Duniani.

72 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Ellen White, alikutana na Henoko huko ambaye naye alikuwa amekwenda kuona maajabu ya Mungu (rejea Early Writings, ukurasa 40).

73 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Fikiria kama nyota zote tuzionazo zina sayari, pengine tisa kama iliyo kwa nyota Jua. Na kila sayari ina watu ambao hawakufanya dhambi, hawafi ni waaminifu kwa Mungu milele, Mungu ana watu wangapi walio upande wake?

74 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mungu anao watu wengi sana walio upande wake.
- Kitendo cha kumtoa Mwana wake pekee ili kutufia ni muujiza wa miujiza.
- Maana angeweza kuangamiza Dunia na kutumia siku sita kuumba nyingine.

75 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mungu alitumia njia ndefu ya kutukomboa kwa kutupa nafasi nyingine ili tuoke, njia ambayo ilisababisha amtoe Mwana wake wa pekee afe kwa ajili yetu.
- Njia ambayo imechukua zaidi ya miaka 6,000 sasa.

76 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Upendo wa Mungu kwetu ni wa ajabu sana, hauwezi kuelezeka au kueleweka kwetu viumbe wake (rejea Yohana 3:16).

77 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mungu ameumba aina tofauti ya nyota, kwa sababu ana uwezo mkubwa na wa pekee.

78 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Biblia ikiongea juu ya aina tofauti ya nyota inasema: ***"Kuna fahari moja ya Jua, na fahari nyingine ya Mwezi, fahari nyingine ya nyota; maana iko tofauti ya fahari hata kati ya nyota na nyota"*** (1Kor. 15:41).

79 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kwa kawaida, umbali kati ya nyota na nyota ni maili trillion 30, kwa tarakimu, 30,000,000,000,000

80 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kati ya nyota na nyota ni maili trillion 30

81 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mpangilio makini wa umbali kati ya nyota na nyota unaonyesha hekima na uwezo wa Mungu.

82 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kwa macho, nyota zinaonekana kama zimekaa bila mpangilio, kumbe zimepangiliwa vizuri ajabu. Mungu ni Mkuu.

83 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Nyota zimepangwa vizuri.

84 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- MWENDO WA NURU
- Nuru ni kitu kinachosafiri kwa kasi zaidi kuliko vitu vyote vinavyojulikana.

85 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Nuru husafiri maili 186,000 kwa sekunde moja. Ni mwendo mkali sana.

86 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kupata umbali ambao nuru husafiri kwa mwaka, itabidi kuzidisha maili 186,000 mara nukta 60 mara dakika 60 mara saa 24 mara siku 365.25 (mwaka mmoja).

87 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mwendo wa nuru kwa mwaka ni sawa na 186,000X60X60X24 X365.25 = maili trillion 5.800,000,000,000.

88 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kwa kifupi, nuru husafiri umbali wa maili trillion 5.8 kwa mwaka. Huo ni umbali mkubwa sana.

89 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kwa kuwa umbali kati ya nyota na nyota ni mkubwa mno, tunauhesabu kwa kutumia miaka ya mwendo wa nuru (Light years).

90 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Tukisema toka nyota hii mpaka ile, ni miaka 10 ya mwendo wa nuru, tuna maana, mwendo wa nuru wa mwaka 1, ambao ni maili trillion 5.8 X miaka 10 = maili trillion 58.

91 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Je, kuna nyota ngapi angani?
- Zipo nyota billion 200 zilizofungwa kwenye uvutano mmoja, na mfungamano wa nyota hizo unaitwa "Galaxy"

92 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Galaxy yetu inaitwa "Milky-Way".
- Nyota zote kwenye galaxy yetu zimeachana umbali wa maili trillion

  30 toka moja hadi nyingine.

93 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- Kipenyo cha eneo ambalo zimeenea ni miaka 120,000 ya mwendo wa nuru, yaani, kama nuru itasafiri kwa maili 186,000 kwa sekunde, itachukua miaka 120,000 kutoka nyota ya mwisho upande huu hadi ya mwisho upande mwingine, Mungu ni Mkuu sana.

94 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mchoro wa mfungamano wa nyota (Galaxy)




95 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kama nyota zote billion 200 zina sayari tuseme 9 na kila sayari ina watu mabilioni ambao hawakutenda dhambi, ni watakatifu kwa Mungu milele, hawafi,Mungu ana watu wangapi walio upande wake? Wengi sana. Akili zetu haziwezi kuelewa.

96 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Daudi alipoangalia vitu alivyoviumba Mungu, alisema: ***"Nikiziangali mbingu zako, kazi ya vidole vyako, Mwezi na Nyota uliozoziratibisha; mtu ni kitu gani hata umkumbuke na binadamu hata umwangalie?*** (Zab. 8:3-4).

97 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kila nyota kwenye galaxy huzunguka katikati ya galaxy kwa mwendo wa kasi bila kusogea nyota nyingine maana kila nyota inazunguka. Kila nyota huzunguka pamoja na sayari zake.

98 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

*SEHEMU YA TATU*
*NA*
- *PR. SULEMANI MANGE*

99 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Daudi anasema: ***"Kwa neno la BWANA mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake"*** (Zab.33:6). Vyote vimeumbwa na Mungu.

100 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Sehemu nyingine Daudi anasema: ***"BWANA ndiye mkuu mwenye kusifiwa sana, wala ukuu wake hautambulikani"*** (Zab. 145:3). Ni kweli ukuu wa Mungu hautambulikani kwa wanadamu, tutakapofika mbinguni, atatufundisha yeye mwenyewe juu ya ukuu wake.

101 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Daudi anaendelea kusema: ***"Kizazi kwa kizazi kitayasifu matendo yake, kitayatanganza matendo yako makuu. Nitaifikiria fahari ya utukufu wa adhama yako, na matendo yako yote ya ajabu. Watu watayataja matendo yako ya kutisha, nami nitausimulia ukuu wako"*** (Zab.145:3-6).

102 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Biblia inasema: ***"Na vilisifu jina la BWANA, kwa maana aliamuru vikaumbwa. Amevithibitisha hata milele na milele, ametoa amri wala haitapita"*** (Zab. 148:5-6). Wale wanaodai kuwa vitu vitafikia mwisho, aliyeviumba anasema amevithibitisha milele na milele. Amina.

103 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Je, kuna mfungamano wa nyota mwingine kando ya huu wa Milky-Way ulio na nyota billion 200? Jibu ni "Ndiyo".

104 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Magharibi mwa nyota inayoitwa Beta, magharibi mwa msalaba wa kusini, kuna mfungamano wa nyota mwingine unaoonekana kwa macho, ulio na nyota billion 200, nao unaitwa Andromeda.

105 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Galaxy ya Andromeda iko umbali wa miaka million 2.2 ya mwendo wa nuru toka galaxy yetu ya Milky-Way.
- Iko mbali sana.

106 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Sasa tumeshaona galaxy mbili, Milky-Way na Andromeda. Kama kila nyota kwenye galaxy hizo (nyota billion 400), ina sayari tisa na kila sayari ina mabilioni ya watu watakatifu, Mungu ana watu wangapi?

107 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Je, kuna galaxy mbili tu alizoumba Mungu, Andromeda na Miky-Way? Jibu ni hapana, Mungu ana galaxies nyingine.

108 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kuna galaxies 25 zikiwemo Andromeda na Milky-Way zilizofungwa kwenye uvutano mmoja na kuunda kitu kinachoitwa: Mfungamano wa Galaxy (cluster of galaxies). Mfungamano huo unaitwa "Local Group cluster of galaxies".

109 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- Kama kuna galaxies 25 na kila galaxy ina mabillion ya nyota na kila nyota ina sayari tuseme tisa na kila sayari ina watu watakatifu wanaomtii Mungu, Mungu ana watu wangapi?

110 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mfungamano wa galaxy - Local Group




111 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Galaxy zote kwenye Local Group zinasafiri kuzunguka katika yake, bila kuleta madhara yo yote.

112 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Je, Kuna mfungamano wa mfungamano wa galaxy mwingine kando ya Local Group ulio na galaxy 25? Jibu ni ndiyo. Maelezo ya maajabu ya Mungu bado yanaelendelea.

113 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Ipo mfungamano ya mfungamano (Clusters of clusters of galaxies) kama Local Group mingine 2,500, iliyofungwa kwenye uvutano mmoja nao unaitwa, VIRGO CLUSTER. MUNGU NI MKUU SANA.

114 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Je, kuna kitu kingine zaidi ya Virgo cluster? Ndiyo, Mungu ni mkuu, nasi hatumjui, ukuu wake hautambulikani.

115 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Kuna vitu kama Virgo cluster viko vingi vilivyofungwa kwenye uvutano mmoja na kuunda kitu kinachoitwa SUPER CLUSTER.

116 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Je, Super cluster ndiyo yote? Jibu ni hapana. Super cluster zipo mamilioni yasiyojulikana idadi yake. MUNGU NI MKUU MNO NASI HATUMJUI. Viona mbali zinampaka haviwezi kuona vyote.

117 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Ukuu wa Mungu hauwezi kufahamika. Biblia inasema: ***"Tazama, hivi ni viunga tu vya njia zake; na jinsi yalivyo madogo manongo'no tusikiayo katika habari zake! Lakini ngurumo za uwezo wake ni nani wawezaye kuelewa nazo?"*** (Ayubu 26:14).

118 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- MAKUNDI YA NYOTA
- Makundi yote ya nyota yako kwenye Galaxy yetu ya Milky-Way na yote ni ya nyota zinazoonekana kwa macho.

119 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Makundi ya nyota ni ya nyota zilizojipanga kwa namna ambayo, zikiungwa kwa mistari, zinaumba umbo fulani.

120 Pr. S. Mange

# Nishani ya Nyota

- 1. Orion (Or), Jina la Kinajimu,The Great Hunter, Mwindaji.
- Kundi hili ni moja ya makundi maarufu sana kati ya makundi 88 yanayotambuliwa na wanajimu. Biblia inaongea juu ya kundi hili.

121 Pr. S. Mange

# Nishani ya Nyota

- Biblia inasema: ***"Je! Waweza kuufungua mnyororo wa Kilimia, au kuvilegeza vifungo vya Orioni? Je waweza kuziongoza sayari kwa wakati wake? Au waweza kuongoza Dubu na watoto wake?"*** (Ayubu 38:31-34)

122 Pr. S. Mange


# Nishani ya Nyota

- Nyota mashuhuri katika kundi la Mwindaji ni: Betelgeuse (700) yaani, iko mbali wa miaka 700 ya mwendo wa nuru.
- Nyingine ni Rigel (900), Bellatrix, Saiph na Nebula, iliyo na tundu katikati.

123 Pr. S. Mange

# Nishani ya Nyota


Mchoro wa Kundi la Mwindaji.




124 Pr. S. Mange

# Nishani ya Nyota

- Nebula ni nyota iliyo na tundu katikati, nyota nyingi sana zina matundu katikati.
- Angalia mchoro huo hapo chini.



**Nyota yenye tundu Dunia inaweza kupita tunduni.**

125 Pr. S. Mange


# Nishani ya Nyota

- 2. Crux (Cru), Msalaba Kusini Southern Cross.
- Msalaba wa Kusini uko Kusini mwa anga na magharibi yake, unaweza kuiona galaxy ya Andromeda. Kuna nyota mbili mashariki yake, Rigel Kentaurus na Hadar.

126 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Msalaba wa Kusini




127 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- 3. Big Dipper, Kata.
- Kundi la Big Dipper huonekana kaskazini mwa anga karibu muda wote, nalo hugeuka geuka. Nyota ya kwanza kwenye kati ya zile nne zinazounda sura ya kata inaelekea ncha ya Kaskazini (Northern pole) daima.

128 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mchoro wa Big Dipper (Kata).




129 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- 4. Gemini (Gem), Twins, Mapacha.
- Kundi hili, liko juu kidogo mwa kundi la Mwindaji. Nyota zake zinafanana na watu wawili waliopiga magoti kuelekeana.
- Nyota mashuhuri ya kundi hili ni Pollux (34), na nyingine ni Castor.

130 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mchoro wa Gemini (Gem), The Twins, Mapacha




131 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- 5. Leo,The Lion, Simba.
- Kundi la Simba liko chini ya kundi la Mwindaji.

132 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota


- Mchoro wa kundi la Simba.




133 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 6. Pleiades, Seven Sisters, Kilimia.
- Kundi hili lina nyota saba nne juu tatu chini



134 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- 7. Canis Major (CMa), The Great Dog, Mbwa Mkubwa.
- Kundi la Mbwa Mkubwa liko chini kidogo ya kundi la Mwindaji. Nyota mashuhuri ya kundi hili ni Sirius (8.6), inang'aa kuliko nyota zote angani.

135 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mchoro wa Mbwa mkubwa.




136 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- 8. Zenith, The Great Triangle, Pembe Tatu Kuu.
- Kundi hili huonekana kaskazini mwa dunia. Nyota zake mashuhuri ni Deneb (1,400), yaani iko umbali wa miaka 1,400 ya mwendo wa nuru, na nyingine ni Altair (16) na Vega (926), Jua huelekea iliko nyota ya Vega.

137 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Zenith, The Great Triangle, Pembe Tatu Kuu.




138 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- 9. Canis Minor (Cmi), The Lesser Dog. Mbwa Mdogo.
- Kundi hili liko chini kidogo ya kundi la Mbwa Mkubwa, Mwindaji ana Mbwa wawili.

139 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mchoro wa Mbwa Mdogo.




140 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- 10. Scorpius (Sco) Scorpion, Nge.
- Kundi la Scorpius, Nge huonekana kusini kidogo mwa anga.
- Nyota mashuhuri ya kundi hilo inaitwa Antares. Ni moja ya nyota kubwa sana, iliyo na kipenyo cha zaidi ya maili milion sita.

141 Pr. S. Mange


## Nishani ya Nyota

- Kama Antares itawekwa mahali ilipo Jua, katikati ya solar sytem yetu, itaenea hadi kufikia orbit ya vimondo, baada ya sayari ya Mars.

142 Pr. S. Mange

## Nishani ya Nyota

- Mchoro wa Kundi la Scorpius - Nge





143 Pr. S. Mange

- 11. Andromeda (And) The Chained Princess.
- Kundi la Andromeda liko karibu na inakoonekana galaxy.
- Nyota inayong'aa zaidi kwenye kundi hili inaitwa Andromedae.

144 Pr. S. Mange

- Mchoro wa Kundi la Andromeda




145 Pr. S. Mange


# Nishani ya Nyota

- 12. Apus (Aps) The Bird of Paradise, Ndege wa Paradiso.
- Kundi hili liko kusini zaidi mwa anga. Kundi hili lilinguliwa na Johann Bayer mwaka 1603, aliyeanzisha matumizi ya herufi za Kigiriki kuziita nyota kwenye kundi kulingana na kung'aa kwake.
- Nyota inayong'aa zaidi inapewa herufi ya alpha.

146 Pr. S. Mange

# Nishani ya Nyota

- Mchoro wa Kundi la Apus, Ndege wa Paradiso.




147 Pr. S. Mange

# Nishani ya Nyota

- Mungu ni Mkuu mno,kila mmoja amche, na kumheshimu katika maisha yake yote.
- Amina

148 Pr. S. Mange